

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO**



TAARIFA KWA UMMA

**UJENZI BARABARA BARIADI HADI MASWA MKOANI SIMIYU WASHIKA
KASI**

UJENZI wa barabara yenye urefu wa kilometa 50 kati ya mji wa Bariadi na Maswa mkoani Simiyu kwa kiwango cha lami, inayojengwa kwa gharama ya shilingi bilioni 88, unaendelea kwa kasi ambapo hivi sasa umefikia asilimia 34.

Kaimu Meneja wa Wakala wa Barabara Nchini-TANROADS, mkoa wa Simiyu, Mhandisi Mohamedi Athumani, ameiambia timu ya maafisa wa Serikali inayoongozwa na Wizara ya Fedha na Mipango, inayofuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo mkoani humo kwamba mradi huo utakapo kamilika mwezi Oktoba mwakani, utafungua fursa za kibiashara na kiuchumi kwenye mkoa huo na mikoa jirani ya Mwanza, Shinyanga, Singida na nchi jirani ya Kenya.

Amesema kuwa kazi zilizofanywa na mkandarasi anayejenga barabara hiyo, Kampuni ya CHICO ya China, ni kuanza kwa ujenzi wa madaraja makubwa mawili ya Simiyu na Banhya na uinuaji wa tuta la barabara maeneo mbalimbli ya mradi.

"Kuna madaraja mengine madogo madogo (*Pipe culverts* 57) pamoja na makalvati madogo (*Box culverts* 12), kwenye kipande hiki cha Barabara chenye urefu wa kilometa 50 na mkandarasi, Kampuni ya CHICO inafanyakazi vizuri na tuna imani kwamba ujenzi wa barabara hii utakamilika ifikapo mwezi Oktoba, 2019 kama mkataba unavyoonesha" alifafanua Mhandisi Athumani.

Kwa upande wake, Mhandisi Mshauri Mkazi wa mradi huo, Mhandisi Swalihi Kazuvi amesema kuwa barabara ya Mwigumbi-Maswa-Bariadi na Lamadi, inayojengwa kwa kiwango cha lami, yenye urefu wa kilometa 172, itakapokamilika, italeti chachu ya maendeleo yanayopitiwa na barabara hiyo.

"Kipande cha barabara ya lami kutoka Mwigumbi mpaka Maswa na kile cha Bariadi hadi Lamadi vimekamilika kwa hiyo kipande kilichobaki ni hiki (Bariadi-Maswa), ndio maana unaona magari yanayopita barabara hii ni mengi licha ya kwamba kipande hiki cha kilometa 50 hakijakamilika, madereva wanaona afadhali wapite huku kwenda Musoma kuliko kupitia njia ya Mwanza" aliongeza Mhandisi Swalihi Kazuvi

Lengo la ziara hiyo ya maafisa wa Serikali ni kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayotekelezawa katika Mkoa huo ili kujua mafanikio, changamoto na mikakati ya kukabiliana na changamoto hizo.

Imetolewa na;

Benny Mwaipaja
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Wizara ya Fedha na Mipango